# *Sauti Ya Mungu Katika Siku Hizi Za Mwisho*

Bila shaka ni majaliwa kurudi miongoni mwa hawa Wahispaniola tena asubuhi ya leo. Nami sijui kama Jim anauchukua huu. Loo, anarekodi. Ningali nina ile sahani ambayo ile kwaya ndogo ya Kihispaniola ilirekodi wakati nilipokuwa hapa siku zilizopita pamoja na Ndugu Garcia. Nami ninasahau ule wimbo mfupi waliokuwa wakiniimbia. Lakini, loo, jinsi nilivyoupenda huo! Na wale watoto sasa wote wamekua na wamefunga ndoa. Ninasikia kutoka kwao mara kwa mara. Na niliingia asubuhi ya leo na kumwona mtoto Joseph, na sasa hili lilinifanyia jambo fulani, na bila shaka nilifurahi kumwona.

2 Na, sasa, nina neno moja ninaloweza kusema katika Kihispaniola. Je! mngetaka kulisikia? "Aleluya!" Kamwe sitalisahau neno hilo. Nilikuwa nikijaribu kumfanya mwanamke mmoja kiziwi kunisikia wakati mmoja. Sasa, huenda nikalitamka hili visivyo, mnaona, bali vizuri kabisa ninavyoweza kukumbuka lilikuwa ni "oiga." Hilo ni sahihi? *Nisikie. Sikia*, "oiga." Halafu kamwe sitasahau, "Gloria a Dios!" Ni ajabu sana! Loo, nilikuwa na nafasi ya kuwa kule chini kwenye mji mkuu, Jiji la Meksiko, kuzungumza nao kule chini. Jinsi nilivyokuwa na furaha! Nami nilikuwa nikininii . . .

3 Nilikuwa huko Finland baada ya mimi kuwa hapa. Na daima inanikumbusha juu ya kuzugumza na maskini mwanamke mmoja wa Kifini. Walinipeleka mpaka mahali wanapoita "bethania." Kila taifa lina wazo lake lenyewe. (Mimi, je! mnapata mwangwi, niko karibu sana na hicho? Mnaweza kusikia vizuri, na hivyo je?) Maskini mwanamke huyu, alikuwa ni mtu mdogo anayependeza sana. Lakini alikuwa ni kama mimi, alipenda kuzungumza sana. Naye mkalimani . . . alizungumza upesi sana, naye—naye mkalimani asingeweza kuyatamka upesi vya kutosha kama vile mwanamke huyo alivyotaka kuyasema. Naye angesimama na uso wake ungegeuka kuwa mwekundu, alisema, "Nawalaumu wale jamaa wa Babeli."

4 Lakini, mnajua, nimeona ya kwamba nde—ndege wote wanaimba katika Kiingereza, mbwa hubweka katika Kiingereza, watoto wachanga hulia katika Kiingereza. Sijui tuna shida gani kwa vyovyote vile. Lakini kila mmoja wetu anafikiri ya kwamba lugha ye—yetu ndiyo itakayokuwa lugha ya ule Utawala wa Miaka Elfu, hakika. Bali sisi ambao tumempokea Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli, sababu tuna lugha ya Kimbinguni.

5 Tunaye Ndugu Rowe pamoja nasi hapa asubuhi ya leo, mwanadiplomasia kutoka Washington. Ninaamini alitumika chini ya Marais watano ama sita, Marais saba. Nanyi mnajua jinsi ninavyojisikia nikisimama hapa, kwenye jukwaa hili, kuzungumza, huku mtu kama huyo ameketi nyuma yangu. Lakini ushuhuda wake daima ulikuwa ni mzuri sana kwangu, na hasa sana wakati yeye. . .Naamini alikuwa ni Mlutheri, kama sijakosea, ama Mkatoliki au Mlutheri, Mlutheri. Naye alisema yeye. . .kitu kuhusu kutambaa chini ya hema kwenye mkutano wa Kipentekoste, naye akaamka. . .Hatimaye akafika madhabahuni, na, alipofika, Bwana alishuka juu yake na kumbariki sana hata. . .Nafikiri anaweza kuzungumza katika karibu lugha saba mbalimbali. Naye alisema alijaribu moja, "haikufaulu," kisha akajaribu nyingine, "haikufaulu." Nami nadhani anaweza kuzungumza Kihispaniola jinsi vile vile ninyi nyote mnavyoweza kuzungumza. Kwa hiyo a—alijaribu zote, wala hazingefaulu. Na, mnaona, mwajua nini, Mungu alikuwa mwema sana, Yeye alishuka na kumpa lugha ambayo hakuwa ameijaribu hapo kabla, kasema, "Inafaulu!" Hiyo ni kweli. Nafikiri hivyo ndivyo itakavyokuwa ng'ambo ya pili.

6 Kumbukumbu nyingi nilizo nazo moyoni mwangu za lile kanisa dogo kule juu, naamini linaninii. . .loo, ninasahau mahali lilipo. Liko hapa mahali fulani karibu na Mtaa wa Tonto. Nami ninakumbuka jambo hilo. Ninaweza kukumbuka neno "Mtaa wa Tonto," mahali ambapo kanisa la Kimitume la Kihispaniola lilipokuwa.

7 Nilikuwa nikimwambia mchungaji, "Hapa pangekuwa ni mahali pazuri sana pa kufanyia uamsho," nafasi tele, kanisa jipya, watu wazuri. Kwa hiyo nafikiri litajiandaa kwa ajili ya uamsho siku moja. Ombeeni jambo hilo, tuje tufanye uamsho. Sasa, natumaini ni marudio tu ya ule tuliokuwa nao kwenye lile kanisa lingine. Ninakumbuka nikisimama uwanjani, nikiegemea uani, huku na huko mitaani, kujaribu kuondoka pale usiku, kwa kweli ulikuwa ni msisimko ambao sijausahau kamwe. Nami nina sa—sahani ya wale mabibi wadogo, wale wasichana na ndugu walioimba na kutoa sahani hiyo. Nao wangejaribu kuimba "Amini Tu," nao hawakuupata vizuri kabisa, unajua. Wangesema, badala ya "amini tu," wanasema "ahamini tu," unaona.

8 Nami ninamkumbuka Rebekah, binti yangu, Sarah, na hata sasa wanasema, "Baba, imba, cheza ile sahani ndogo ya maskini. . ." Badala ya kusema "Spanish," wasingeweza kulitamka neno hilo, walisema, "wasichana wa Spinachi, wasichana wadogo wa spinachi wakiimba 'Amini Tu.'"

9 Vema, ninakumbuka waliufuatilia mkutano huo. Uamsho ulikuwa ukiendelea wakati huo, nao waliufuatilia mkutano huo kote hata Pwani ya Magharibi. Nami. . .kitu kidogo kilitia nanga moyoni mwangu tulipoondoka California, mimi

pamoja na Ndugu Moore, na Ndugu Brown, huko juu kabisa kwenye makao makuu. Na wakati niliposhuka kupita kwenye jengo hilo usiku huo, watoto hao wakisimama hapo wakiimba huo, “Yeye anakujali.” Mmeusikia. “Kupitia kwenye jua ama vivulini, Yeye hukutunza.” Mara nyingi katika nchi za ng’ambo, kwenye viwanja vya vita vya ugomvi wa ulimwengu, nikijaribu kuuleta Ujumbe wa Kristo, ningewakumbuka wasichana hao na wavulana wakiniimbia wimbo huo, “Yeye anakujali. Kupitia kwenye jua ama vivulini, Yeye angali anakujali.” Kwa hiyo huo umekuwa ni uvuvio mkuu, ni msaada.

10 Kuonana na mchungaji wenu mzuri, na nina furaha sana kuona ya kwamba kanisa liko hai nanyi mna jengo hili kubwa na zuri hapa, likienea wote, nafasi kubwa ya kuegeshea magari. Mahali halisi tu mikononi mwa Roho Mtakatifu, kama tukiweza tu kumfanya apaone na ajue ya kwamba tunauombea uamsho. Yeye, ninaamini angeweza kutoa mmoja.

11 Sasa, usiku wa leo tuko kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, lile kanisa la Jina la Yesu, ng’ambo ya pili. Naye Ndugu Outlaw, ninaamini katika . . . ni kanisa la Apostolic, pia. Ninafikiri yeye aliita tu jina lake, hilo kanisa, Jina la Yesu. Ninafikiri yeye ni wa imani ya kiapostolic. Na kwa hiyo tunapaswa kuwa huko usiku wa leo. Na sasa hatuliambii kanisa hili la Kihispaniola, “sasa njoni kule,” kwa sababu mnakaa kwenye wajibu wenu. Na kisha kutakuwako na mkutano mkubwa wa Wafanya Biashara Wakristo, unaoanza Alhamisi, baada ya ibada kufungwa katika makanisa mengine, Alhamisi. Na mkutano huu, watakuwa na wahubiri wazuri sana, na kwa hiyo Oral Roberts, na ndugu mmoja wa Kimethodisti ambaye ndio kwanza aokolewe, nao wanadai ya kwamba yeye ni mhubiri hodari sana. Nami nina hakika mtaifurahia mikutano hii. Nanyi watoto matineja, wana mkutano kule wa matineja pia, kama vile ndugu alivyotangaza sasa hivi. Nitawapeleka watoto wangu kule ili kwamba waweze kuuhudhuria huu. Na kwa hiyo sasa karibuni, tutafurahia kuwa nanyi. Bwana awabariki nyote.

12 Na sasa ninataka kufungua katika Biblia na kusoma sehemu ya Neno Lake lililobarikiwa. Nami nimechagua asubuhi ya leo, kwa kitambo kidogo, sitaki kuwashikilia kwa muda mrefu sana, fungu la maneno, na moja la hayo linapatikana katika Samweli I, hilo lingine linapatikana katika Isaya. Nami ningetaka kusoma kutoka katika Isaya kwanza. Nami . . .

13 Mwaweza kusikia vizuri, kila mahali? Katikati ya maikrofoni hizi, zinaonekana kwangu kuwa zina nguvu sana kushika, sijui ni kwa nini. Mnasikia vizuri huko, inua mkono wako. Vema, vema.

14 Sasa, mimi kidogo tu nimepwelewa na sauti, bila shaka, hiyo ni kutokana na kuzungumza sana. Na tangu nilipokuwa hapa pamoja na hawa ndugu wa Kihispaniola, yapata miaka kumi

na sita iliyopita, nakisia, labda karibu miaka kumi na sita ama kumi na saba iliyopita, vema, nimekuwa nikihubiri tangu wakati huo. Kwa hiyo nilikuwa nimechoka basi, nikasema, nami ningali ni mchovu, bali ningali ninaendelea kwa neema ya Mungu.

15 Sasa hebu na tufungue Isaya 40, mlango wa 40 wa Isaya; na mlango wa 1, ama mlango wa 3 wa Samweli I. Na wakati tumeshikilia mahali hapo kwa ajili ya kusomwa kwa Neno, ningetaka sisi tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo wa maombi.

16 Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru leo kwa ajili ya fursa hii ya kusimama kwenye madhabahu hii ya kupendeza ambayo imewekwa wakfu kwa Mungu na kwa ajili ya kazi Yake. Na kama tunavyojua ya kwamba watumishi Wako wamesimama nyuma ya jukwaa hili hapa ama mimbara mara nyingi, na wakiwa ni wenye maisha yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi Wako.

17 Na kwamba *hili*, asubuhi ya leo, linaleta kumbukumbu, kumbukumbu za uamsho ambao ndio kwanza ulikuwa ukianza, pamoja na Roho Mtakatifu aliyekuwa ameshuka katika umbo la Nuru kuu, kama Nguzo ya Moto, na akasema ya kwamba Ujumbe huu utaenea kote ulimwenguni. Na sasa leo hii hiyo ni historia. Ujumbe huu umeshika moto kupitia kwa watu mashuhuri, baada ya kuuona, kama vile Oral Roberts na Tommy Osborn, na Tommy Hicks na wengine wengi. Na kwa jitihada ambazo tumeweka pamoja, tunaona Ujumbe huu umeiwasha mioto ya uamsho katika kila taifa chini ya Mbingu, wa Ujumbe wa kipentekoste. Kwa jambo hili tunatoa shukrani na sifa Kwako, Ee Mungu Mwenye Nguvu.

18 Na sasa leo tunaomba ya kwamba Wewe utauandaa moyo wetu, kujifanya tayari kwa ajili ya Unyakuo mkuu utakaotukia hivi karibuni, tunaamini. Na endapo mioyo yetu haiko katika hali nzuri kwa ajili ya jambo hilo ama kwa chochote kile ulichotuwekea akiba, tunaomba utusamehe kwa kupungukiwa kwetu, Nawe utasema nasi leo kupitia kwenye Neno Lako. Mbariki mchungaji wa kanisa hili, mashemasi wake, wadhamini, na wafuasi wote, washiriki. Bariki kwaya hii ndogo, na mpiga piano, wanamuziki. Kwa jumla, wabariki wale wanaoingia malango ya mahali hapa. Jalia waondoke wamebadilishwa kila wakati, wakiwa karibu zaidi na Wewe kuliko walivyokuwa walipoingia. Tujalie, Baba. Na jalia jambo hilo liwe hivyo, hata asubuhi ya leo, kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

19 Sasa tukifungua Kitabu cha Isaya, mlango wa 40, tunasoma.

> *Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu, asema . . . Mungu.*
>
> *Semeni* maneno ya faraja kwake *Yerusalemu, kauambieni kwa sauti kuu ya kwamba vita vyake vimekwisha, uovu wake umeachiliwa; kwa kuwa*

*amepokea kwa mkono wa Bwana adhabu maradufu kwa dhambi zake . . .*

*Sikilizeni, ni sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya Bwana; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu.*

*Na kila bonde litainuliwa, na kila mlima na kilima kitashushwa; palipopotoka patakuwa pamenyoka, na palipoparuza patasawazishwa;*

*Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya.*

Sasa katika Kitabu cha Samweli, Samweli I, mlango wa 3, ninataka kusoma aya ya 1, ya 2, na ya 19.

*Basi mtoto Samweli akamtumikia Bwana mbele ya Eli. Na neno la Bwana lilikuwa adimu siku zile; hapakuwa na mafunuo dhahiri.*

*Ikawa wakati huo, Eli alipokuwa amelala mahali pake tena macho yake yalikuwa yameanza kupofuka, hata asiweze kuona;*

*. . . taa ya Mungu ilikuwa haijazimika bado, na Samweli alikuwa amelala katika hekalu la Bwana, palipokuwa na sanduku la Mungu;*

*Basi wakati huo Bwana akamwita . . . naye akasema, Mimi hapa.*

Aya ya 19.

*Samweli akakua, naye Bwana alikuwa pamoja naye, wala hakuliacha neno lake lo lote lianguke chini.*

20 Loo, hilo lingekuwa ni fungu la maneno la kutosha ambalo tungeweza kuzungumzia hapa kwa mwezi mzima, nasi tungepata miktadha mingi kutoka kwenye fungu hili tukufu la maneno. Lakini asubuhi ya leo, nasi tuna yapata tu dakika ishirini kutoka katika wakati mzuri kutoka kwenye ninii yetu . . . Nadhani shule ya Jumapili imekwisha ama labda inaifuata hii, sijui. Bali, hata hivyo, ninataka kutumia fungu la maneno la, *Sauti Ya Mungu Katika Siku Hizi Za Mwisho*.

21 Ni wakati mzuri sana. Tunatambua ya kwamba mahali tunapozungumzia katika Maandiko, ya kwamba imesema, “Hapakuwa na mafunuo dhahiri katika siku za Samweli.” Kwa hiyo, “Mahali pasipo na maono,” Biblia ilisema, “watu huangamia.” Hatuna budi kuwa na ono. Na maono huwajia manabii, na ni Neno la Bwana lililonenwa kwao.

22 Nasi tunaona ya kwamba Eli hakuwa nabii, Eli alikuwa ni kuhani. Naye alikuwa anazeeka, na macho yake yalikuwa yakififia, wala asingeweza kuona apate kutembea-tembea,

alikuwa ni mtu mzito sana. Naye alikuwa ameanza kuacha kazi ya Mungu ipite bila kushughulikiwa.

23 Na jambo hilo ni kama ilivyo siku hizi. Ninafikiri kanisa, shirika na madhehebu, yamekuwa hudumani kwa muda mrefu sana, na yanaanza kulegea. Na kazi ya Bwana inaachwa bila kufanywa, Neno la Kweli, kwa sababu kanisa, lenyewe, limepofuka. Nasi tunahitaji, leo, Sauti ya Mungu kuzungumza miongoni mwetu, kuturudisha.

24 Na, unaona, Eli alikuwa amelala, na ninii . . . macho yake yalikuwa yakififia. Yeye alikuwa ni kuhani. Nao hawakuwa na maono dhahiri kutoka kwa Bwana. Na hiyo haja kubwa!

25 Naye Mungu ameahidi kukidhi mahitaji ya wakati upaswao. Yeye daima hufanya hivyo. Nasi tunahitaji Sauti ya Mungu leo, kukidhi mahitaji ya wakati upaswao, kukabiliana na wakati tunaoishi. Na baada ya Yeye kuahidi jambo hilo, tunaweza kuwa na hakika ya kwamba Yeye atatimiza ahadi Yake. Huo ndio ujasiri ambao mwaminio anao katika Muumba wake, ya kwamba Yeye aliahidi kukidhi mahitaji.

26 Na, leo hii, sababu moja ambayo kanisa liko katika hali lililomo, ni kwa sababu ziko sauti nyingi sana, sauti zingine nyingi sana kulivutia kanisa kutoka kwenye Sauti ya Mungu, mpaka kuna shaka sana kwamba wengi wangeisikia Sauti ya Mungu ingawa ilinena moja kwa moja katikati yao. Labda hata wasingeielewa, kwa sababu ingekuwa ni kitu kigeni kwao. Wamejikoleza sana kwenye sauti za siku hizi!

27 Na kama tukiangalia, katika somo letu la Maandiko, ya kwamba Sauti ya Mungu ilikuwa ni ya kigeni kwao.

28 Na imekuwa tena hivyo leo, ya kwamba Sauti ya Mungu . . . Zipo sauti zingine nyingi sana. Na basi kama Mungu aliahidi angetupa Hiyo, na endapo sauti zingine ni kinyume na Sauti ya Mungu, basi haina budi kuwa ni sauti ya adui wetu, kutuchanganyisha, kusudi tusiifahamu Sauti ya Mungu wakati ikinena.

29 Nasi tunaona kilikuwa ni kitu kinachofanana na kile cha Eli na Samweli, bali Eli alitambua mara moja ya kwamba ilikuwa ni Mungu. Na ilikuwa kabisa ni—ni kukufuru kwa yeye Eli. Kwa sababu, Sauti ya Mungu, ikinena na Samweli, ilikuwa imemwambia kuhusu makosa ya Eli, kwa sababu alikuwa amewadekeza wanawe, nao walikuwa wakichukua fedha na—na nyama kutoka katika sadaka. Hilo halikuwa ni jambo zuri. Nao walikuwa wakifanya makosa, kinyume na Neno la Mungu.

30 Naye Samweli alikuwa na . . . jambo pekee ambalo Samweli angaliweza kufanya, ni kusema dhahiri. Naye alikuwa kidogo anasita kufanya hivyo, kwa sababu jambo hilo lilikuwa linapinga mambo ya mahali alipokuwa amepelekwa akalelewe, Eli na katika hekalu. Lakini Eli alisema, “Sema tu.” Unaona? Naye akamwambia kile hasa kingetukia, ya

kwamba Samweli . . . ama, “Siku za Eli zilikuwa zimekwisha, kama kuhani,” kwa sababu Mungu alikuwa amenena, na Mungu alikuwa akiutuma Ujumbe Wake kupitia kwa nabii Samweli. Kuzaliwa kusiko kwa kawaida kabisa, amewekwa wakfu kwa Bwana tangu utotoni. Mungu alinena naye, kama mtoto, na alikuwa akimwandaa kwa ajili ya kazi iliyokuwa mbele yake. Nao wakati wa Eli ulikuwa unakwisha.

31 Zipo sauti nyingi sana duniani leo, hivi kwamba ni jambo gumu sana, kwa sababu linafifisha Sauti ya Kimbinguni. Kuna sauti nyingi sana za kiakili, sauti kuu sana za watu maarufu ambao ni wasomi kweli kweli, ambao, katika hali za bongo zao, hata wanayatikisa mataifa. Hao si akina yahe, bali wanayatikisa mataifa, wakiyaleta mashirika makubwa pamoja, mikutano mikubwa, ya madoido. Na mtu angechanganyikiwa kidogo. Inatosha kuwachanganya, jinsi mambo haya yanavyoendelea na kufanikiwa. Na kuna sauti ambazo—ambazo huinuka na kuyafanya mambo haya, na zinaifanya Sauti ya Mungu kuwekwa huko nyuma mbali mahali fulani, Sauti ya kweli ya Mungu.

32 “Na Sauti ya Mungu,” wao wanasema, “tutajuaje ni Sauti ya Mungu?” Kwa sababu, kwa maana siku hizi . . . Zamani hizo ilikuwa katika nabii aliyethibitishwa. Sasa, leo hii, jinsi tunavyojua ni Sauti ya Mungu, ni kwa sababu ni dhihirisho la Neno la nabii. *Hili* ndilo nabii wa Mungu. Na Sauti ya kweli ya Mungu humrudisha tu yule Mungu halisi, aliye hai, wa Kimbinguni, pamoja na Neno Lake la Kimbinguni, pamoja na madhihirisho ya Kimbinguni ya Neno la Kweli. Ndipo tunajua ya kwamba ni Sauti ya Mungu. Kwa sababu, na hiyo ya Kimbingu- . . . Kuna nyingi sana katika milki zingine, ambazo karibu huififisha Hiyo kabisa. Lakini, kumbukeni, itameremeta, itajitokeza! Itafanya hivyo.

33 Sasa, kuna sauti leo katika ulimwengu wa siasa. Hiyo ni sauti kuu. Nao watu, kabisa, katika siku hii kuu ya siasa, wataninii . . . Mambo yamechanganyikana katika makanisa yao na kila kitu. Na mara nyingi, kama tulivyoona hivi karibuni, ya kwamba sauti ya siasa kwa kweli ina nguvu kuliko Sauti ya Mungu katika makanisa, vinginevyo Wamarekani kamwe wasingalifanya kile wamefanya karibuni. Unaona? Kamwe wasingalilifanya. Kama Sauti ya Mungu ingalidumishwa ikiwa hai kanisani, kamwe wasingalifanya makosa hayo. Bali sauti ya siasa ina nguvu sana duniani siku hizi kuliko Sauti ya Mungu, mpaka watu wakauza haki yao ya mzaliwa wa kwanza ya Kikristo kwa takataka ya kupendwa na watu, elimu, na nguvu za kisiasa. Ni aibu sana kuona jambo hilo. Kitu kile kile kilicholiunda taifa letu, kile ambacho limejengwa juu yake, watu waligeuka moja kwa moja na—na kupiga kura kuingiza kitu tulichoachia ile nchi nyingine. Na ninii—na Plymouth Rock, na Mayflower na hao wengine, walikuja hapa na—na kuanzisha uchumi huu mkuu tulio nao. Ni kitu kile kile tulichopiga vita vikali tupate kutoka kwake,

tumejirudisha moja kwa moja kwenye makucha yake, kwa kuwa kwamba Biblia inasema ingekuwa hivyo.

34 Na mfumo wa Eli: kuhani badala ya nabii. Nabii ni Neno. Na kuhani alikuwa ni kanisa.

35 Na imefikia mahali ambapo mpaka ikaanza kulegea sana hata Neno ni geni kwa watu. Hawalipati. Kwa hiyo unaweza kulinena, na wala hawalifahamu, kwa sababu hawajafunzwa kulifahamu Hilo. Paulo alisema, "Baragumu ikitoa sauti isiyo dhahiri, ni nani atakayejua kujiandaa kwa vita?"

36 Watu wamefunzwa kuitambua sa—sa—sauti ya kanisa, baragumu ya kanisa, "Tuna wengi zaidi kwenye shule yetu ya Jumapili kuliko hao wengine walivyo nao." Hilo halimaanishi kitu. "Tuna wengi katika dhehebu letu kuliko hao wengine walio nao. Sisi ndio kubwa zaidi miongoni mwa madhehebu." Unaona, hiyo ndiyo aina ya sauti ambayo watu wamefunzwa kufahamu. Mtaani, wao wanatoka kwenda kuwaleta watu na kuwaingiza ndani. Makumi elfu mara maelfu katika kampeni kubwa, kuwaingiza. Wao wana shauku ya nini? "Tuna kanisa lililo kubwa zaidi ya yote. Tuna kusanyiko lililo kubwa kuliko yote. Tuna shule ya Jumapili iliyo na washiriki wengi kuliko zote. Tunaye meya wa jiji ambaye huja kuhudhuria kanisani mwetu." Hayo yote yanaweza yakawa ni mazuri, bali kama kanisa lilo hilo halijafunzwa kuisikia Sauti ya Mungu, Parapanda ya Injili, inafaa kitu gani?

37 Na wakati kitu kikizuka kama kilichozuka katika serikali yetu, kulitukia nini? Kanisa halikujua Sauti ya Baragumu, wala hawakujua la kufanya. Ile ahadi kuu ya ufanisi, jitu la kielimu likiingia, nao wakapita moja kwa moja juu ya kitu kile kile ambacho Biblia ilibashiri, na kuliingiza ndani. Unaona, sauti ya siasa! Na ilithibitisha ya kwamba iliishinda Sauti ya dini, vinginevyo kamwe wasingalifanya kile walichofanya, Sauti ya Injili. Kwa sababu tumeahidiwa mambo mengi sana, tumeahidiwa ufanisi, na hapana shaka tutaupata.

38 Lakini, hata hivyo, hilo halimaanishi chochote kwa mwaminio. Fungueni katika Kitabu cha Waebrania, kwenye mlango wa 11, msikilizeni huyo Mtakatifu Paulo akinena, jinsi ambavyo wao, katika zile siku, "Walizunguka-zunguka katika ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, hawana mahali, wasingeingia jijini."

39 Nilikuwa nikisoma juu ya lile Baraza la Nikea, wakati hoja kuu zilipotokea kule Nikea, Urumi, miaka mia tatu baada ya kufa kwa Kristo, katika lile Baraza kuu la Nikea, wakati lile kanisa kuu lililotetea yaliyokuwa ni ya kweli, walitaka Biblia. Nao waongofu wa Kirumi wa kanisa la kwanza la Kirumi walikuwa wameingiza kanuni za imani, kusema, kwa mfano, kama vile tulivyo na Krismasi.

40 Krismasi, Kristo hakuzaliwa kwenye siku ya ishirini na tano ya—ya Desemba zaidi ya vile mimi nilivyozaliwa siku hiyo. Mbona, milima ya Uyahudi ilikuwa imejaa theluji, na Yeye. . .Ni kinyume na nabii zingine zote za Biblia. Yeye alizaliwa kwenye msimu wa kuchipua majani, kama vile wana-kondoo wote wanavyozaliwa. Kwa nini alizaliwa kibandani badala ya nyumbani? Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo. Kwa nini Yeye hakupelekwa mbio madhabahuni ama kwenye madhabahu Yake ambako alipigiliwa misumari, msalabani? Yeye aliongozwa akapelekwa msalabani. Unamwongoza mwana-kondoo machinjioni. Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo. Kwa hiyo alizaliwa wakati wana—kondoo walizaliwa.

41 Lakini, unaona, kufanya jambo hilo, walikuwa na siku ya kuzaliwa kwa mungu jua, ambayo, kwenye mfumo wa jua, ju—jua katika zile siku tano kutoka Desemba ishirini hadi Desemba ishirini na tano, karibu hakuna kusogea hata kidogo, kwa jua. Lina—linabadilika kidogo kila siku, inaendelea kuwa ndefu na ndefu na ndefu mpaka inafikia siku iliyo ndefu sana katika Julai. Halafu basi, katika Desemba, ndiyo siku iliyo fupi sana. Na ndipo wakati huo mfupi wa tarehe ishirini na tano, kuanzia tarehe ishirini hadi ishirini na tano, walikuwa na sarakasi za Kirumi na sherehe ya siku ya kuzaliwa kwa mungu jua. Ndipo basi Jupita, ambaye alikuwa ni mungu wa Kirumi, ndipo basi waliingiza hilo, katika kusema basi, "Tutachukua siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu na siku ya kuzaliwa kwa mungu jua, tuziweke hizo pamoja ziwe ni sherehe moja kuu." Hilo ni kinyume! Na, loo, miingizo mingi waliyoiweka mle ndani!

42 Ndipo basi wakati watu wa kweli wa Mungu ambao walitaka kudumu na Neno, kama vile Polycarp, Ireneo, Martin, hao watu mashuhuri watakatifu wa mwanzoni, waliotaka kudumu na ile Kweli. . .Na wakati walipoletwa wapitie kwenye hilo Baraza la Nikea, baadhi ya watu hao walikuwa wamekataliwa mpaka manabii wakaja kutoka nyikani bila kitu chochote kilichowafunika ila kipande cha ngozi ya kondoo, kuketi kwenye baraza hilo. Lakini walijua Neno la Bwana. Bali kupendwa na watu, hizo siku kumi na tano za siasa za umwagikaji wa damu, na wakakataliwa. Ndipo tukawa na miaka elfu moja ya wakati wa giza, unaona.

43 Lakini Mungu aliahidi ya kwamba Baragumu hiyo ingelia tena. Daima watu husikiliza Sauti ya kweli ya Neno, daima chunguza kile unachofanya kwa Neno.

44 Sauti ya siasa. Nasi huku Marekani na kote ulimwenguni, tuna sauti kubwa inayonena siku hizi, na hiyo ni sauti ya Hollywood. Imeuteka ulimwengu. Hebu mtu fulani atoke Hollywood na kitu fulani, utakiona kote nchini. Sasa, tunaona ya kwamba wameanzisha mtindo kwa ajili ya wanawake wetu, juu ya nguo zao, mtindo wao wa nywele. Wanabuni vazi hilo.

45 Kanisa linapaswa kujua Sauti ya Baragumu ya Mungu juu ya jambo hilo! Bali kuna kuchanganyikiwa kwingi sana kwa sababu unaona wengine wakifanya hivyo, mifano. Usijilinganishe na mfano wa jinsi hiyo, kwa sababu unaharibika. Daima isikie Sauti ya Mungu, kile anachosema juu ya jambo hilo.

46 Halafu tunaona, huko Hollywood, wanayainua mambo. Na hebu nizungumze kwa dakika moja tu kuhusu jambo hili kabla hatujaenda mbele zaidi. Kulikuwako na ja—jambo lililotokea si muda mrefu uliopita, ya kwamba m—mtu mmoja huko Hollywood. . . Sina neno dhidi ya mtu huyo sasa, yeye ni mwanadamu aliyefiwa na Kristo, bali ni kuwaonyesha tu. Walibuni kitu kidogo kinachoitwa, watoto walikuwa wakikiita "uringe-bayoyo," uringe-bayoyo, ama kitu fulani. Na kama ulipata kuona ukosefu wa uadilifu na mambo yaliyolifuata kundi hilo, katika watoto wadogo. Hilo si sahihi.

47 Sasa, Hollywood i—imejaa wapiganaji wa bunduki. Sasa, mtu yeyote anayejua historia, anajua ya kwamba hao watu huko nyuma katika siku hizo, waliokuwa wapiganaji wa bunduki kama jamaa ha—hao mbalimbali, hawakuwa ni wananchi wema, walikuwa ni maharamia, walikuwa kama Al Capone na Dillinger. Wana mchezo wa Hollywood wanaouita, kwenye—kwenye televisheni, wanaouita, "Moshi wa bunduki." Nami nilisikia kwenye *Monitor* hivi majuzi ya kwamba jamaa anayeucheza, Arness ama kitu kama hicho, ama Arness, ama nasahau jina lake ni nani, naye anapaswa kuchukua. . . Yeye anamwakilisha Matt Dillon ambaye alikuwa liwali huko Kansas. Naye Matt Dillon alikuwa manjano kama sungura. Aliwapiga risasi watu ishirini na wanane mgongoni, watu wasio na hatia, akienda nje ya Jiji la Dodge na kuwavizia kichakani. Ndipo mtu alipopitia hapo, mtu fulani angemwita na kumwambia ya kwamba kulikuwako na haini fulani aliyekuwa akipitia hapo, ndipo anakaa huko nje na, mtu huyo alipoingia, angempiga risasi mgongoni. Sasa tunaona ya kwamba yeye ni "jamaa mkubwa" anayeshuka kuja huko. Mbona, ni—ni kuitukuza dhambi kabisa. Lakini watoto wadogo wa nchi yetu wanaweza kukwambia mambo zaidi juu ya Matt Dillon kuliko wanavyoweza kukwambia juu ya Yesu Kristo. Ma—ma—maduka, maduka ya senti kumi, na idara ya nguo, imejaa wanasesere wengi wa—wadogo wa bunduki, pamoja na kofia ndogo ambazo—ambazo ungeweza kuzinunua mahali popote. Ni sawa kuvaa hizo, bali nina—ninawaambia tu, mnaona. Ndipo wao—wao, ulimwengu wa biashara, unakiokota kitu hicho na kupata mamilioni ya dola kwake.

48 Tuna kile tunachoita "Siku ya Mtakatifu Patrick," tuna kile tunachokiita hizi "sikukuu za dini." Nao ulimwengu wa biashara umeichukua, nao wanapata mamilioni ya dola. "Siku ya Mama," lundo la maua. Mbona, kila siku inapaswa kuwa ni siku ya

heshima kwa mama. Yeye ametoka ameenda mahali fulani, mkongwe, nenda kamwone. Hilo litakuwa na faida kubwa sana kuliko maua yote ungaliweza kumtumia, ama chochote kile. Unaona, bali wanaichukua. Ni sauti, na—nasi tunaungana moja kwa moja nayo. Kwa kweli si sahihi. Lakini utafanya nini? Unaona, tuna—tuna ninii tu . . .

49 Ninajaribu kufikia mahali fulani hapa kuwaambia jambo fulani, kile ni—ninachoamini. Sauti ni adimu, Sauti ya Mungu.

50 Sasa, tunaona ya kwamba waliongoza njia. Na je! mliweza kuona, wavulana wetu wadogo wamekuwa "Ricky" na "Elvis." Kama una mtoto anayeitwa kwa jina hilo, libadilishe upesi sana, mwite namba "moja" ama "mbili," ama chochote kile. Usininii, hilo ni la kuchukiza sana . . . Unasema, "Jina linaleta tofauti gani?" Mbona, hakika, linamaanisha jambo fulani. Jina lako linaonyesha tabia za maisha yako. "Sasa, Ndugu Branham, wewe uko katika elimu ya namba." La, sivyo! Niko kwenye BWANA ASEMA HIVI! Mbona wakati Yakobo, yeye aliliishia jina lake, kama—kama mdanganyifu, mwizi, Yakobo. Na wakati Mungu alipombadilisha, Yeye alilibadilisha jina lake. Mungu alimbadilisha Sauli akawa Paulo, Simoni akawa Petro. Hakika, lina jambo fulani. Na Ricky na Elvis, na majina kama hayo, ni majina ya kisasa ya Marekani ambayo humtupa mtoto moja kwa moja katika kitu hicho. Mnaona ninalomaanisha?

51 Sasa, natumaini sininii . . . Afadhali nirejee nyuma wala nisifuatilie jambo moja zaidi hapa, (mnaona ninalomaanisha?) hata msifahamu. Lakini mambo haya yote hata hayafahamiki na mtu wa kawaida. Hawalipati, kwa sababu wana mwelekeo mmoja. Hayo tu ndiyo wanayosikiliza, sauti hizo.

52 Kuna sauti ya wanafalsafa, Ukomunisti, zinazoahidi jambo fulani ambalo hawawezi kulidumisha. Na hata hivyo asilimia kubwa ya Wamarekani wamenaswa na Ukomunisti. Sasa, nimekuwa katika Ukomunisti, maeneo ya Ukomunisti, hasa, huko Ujerumani, mashariki mwa Berlin. Walikuwa na nyumba kubwa mno za kuonyesha ulimwengu wa nje. Unapaswa kutembea ndani ya hizo, hata hazijamalizika. Ni uchumi wa uongo, wanajaribu kusukumiza jambo fulani.

53 Na, huko Urusi, mahali Ukomunisti ulipozaliwa . . . Ambapo, miaka mingi iliyopita, wakati nilipokuwa mhubiri mvulana tu, labda miaka thelathini na mitatu iliyopita, wakati Unazi, Ufashisti, na Ukomunisti ulipokuwa ukiinuka, nilisema, "Ninanena katika Jina la Bwana! Zote zitaishia kwenye Ukomunisti." Lakini, je! ulipata kuwazia, Mungu ametuachia njia ya kutokea, kama tu tukiichukua. Kuna asilimia moja tu ya Urusi ambayo ni Ukomunisti, asilimia moja, bali ndiyo asilimia inayotawala. Asilimia moja ya Ukomunisti . . . asilimia moja ya Urusi ni Ukomunisti, hasa, bali wanatawala.

54 Na jambo lile lile, Hollywood ni mahali pamoja, bali hao ndio wana nguvu.

55 Yapata theluthi moja ama mbili za watu wa Marekani huenda kanisani, nao ni wafuasi wa kanisa, bali wanatawala katika hayo madhehebu.

56 Kile Ukomunisti unachohitaji kule ni Sauti ya Mungu iinuke miongoni mwao, Nayo ingeuaibisha.

57 Huko Finland, wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa katika wafu siku ile, nao walikuwa wakinileta kutoka miraba mitatu, mahali jamaa huyu mdogo alipofufuliwa, mfu; askari wa Kikomunisti, Warusi, wakisimama pale wakiwa na saluti ya Kirusi, na machozi yakitiririka mashavuni mwao. Wao walisema, "Tutampokea Mungu ambaye anaweza kuwafufua wafu." Ni kutojali kwa kanisa Katoliki na kanisa la Kilutheri, na madhehebu hayo yote, na wamechukua fedha zote, na kujenga mashirika, na bila kuwapa watu kitu chochote. Wanaishi kama watu wengine. Hapana budi kuwe . . .

58 Kile Urusi inachohitaji ni nabii aje jukwaani akiwa na Neno la Bwana, ambalo linaweza—linaweza kukifunga kinywa. Ndipo hiyo asilimia tisini itachukua mamlaka.

59 Kile Marekani inachohitaji ni Sauti ya nabii wa Mungu, ambaye angeweza kusimama na kuilaani Hollywood, na kuyalaani mambo haya katika Jina la Yesu Kristo, ndipo Kanisa la Roho Mtakatifu litashika hatamu. Kuchanganyikiwa kwingi kupita kiasi, unaona, sauti nyingi kupita kiasi zinazoipinga.

60 Kanisa, sauti yake, kila moja linataka wafuasi zaidi. Wabaptisti wanawataka wote, Methodisti inawataka wote, Presbiteri. Sote tuna hizi. Na Katoliki inaonekana kana kwamba itawachukua wote, nao watawachukua. Hiyo ni Sauti ya Mungu hasa kutoka kwenye Biblia hii. Watatawala.

61 Bali Mungu Aliye Juu Sana hatimaye atatawala. Watakatifu watachukua mamlaka, siku moja, Biblia ilisema hivyo. Watachukua mamlaka.

62 Sauti nyingi mno namna hiyo! Kisha kuna sauti ya nabii wa uongo. Hiyo ni sauti mbaya sana, mtu anayejiita nabii. Nabii, bila shaka, ni mhubiri. Neno la kisasa "nabii" kweli linamaanisha "mtu anayehubiri chini ya uvuvio." Yupo mtu anayesimama na kujiita nabii, na kulikana Neno la Mungu, anakanusha Ukweli wa Mungu. Zipo sauti nyingi sana!

63 Muda mfupi tu uliopita, kulikuwako na ndugu kule nje akinionyesha mahali pa kuja huku, bali mimi . . . nafikiri alishangaa ni kwa nini nilienda juu barabarani kisha nikageuka na kurudi. Kama upo hapa, ndugu, nilikuwa nikisikiliza kitu fulani, ilikuwa ni ndugu ze—zetu weusi, wale wanegro. Wana hekalu hapa, nao wanaliita, "Eliya Mohammed," ama kitu kama hicho, "Eliya Mohammed mdogo." Wakiinuka na sauti,

na kusema ya kwamba wao ndio sauti itakayowatoa jamii ya watu we—weusi kutoka kwenye machafuko haya. Hilo, mnaona, jambo lenyewe, Uislamu wao—wao—wao uko hapa, Msikiti wao. Mbona, hivi hamwoni, ya kwamba msingi wake wenyewe, ni mbaya!

64 Watu weusi, kama tu vile watu weupe, watu wa hudhurungi, na watu wa manjano, sio kurudi—kurudi kwenye Uislamu, bali kumrudia Kristo, kanuni zenyewe ambazo Biblia inafundisha. Uislamu unalipinga Neno. Sasa, nilikuwa na majaliwa ya kuwaongoza Waislamu elfu kumi kwa Kristo wakati mmoja huko Durban, Afrika Kusini. Hautoi kitu ila saikolojia. Nayo saikolojia ni sawa mradi tu saikolojia hailikani Neno. Bali wakati saikolojia inapolikana Neno, basi saikolojia ni makosa. Inatoa sauti isiyo dhahiri. Kila kitu kitapita ila Neno la Mungu, Yesu alisema hivyo, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Kwa hiyo, unaona inatubidi tudumu na Neno, ile Sauti.

65 Wengi sana huchanganya mambo! Watu wanaamka, hawalijui Neno, nao wanasema mambo, na labda jambo linasikika ni la maana sana. Ukomunisti ni kitu cha maana sana, "Kila mtu ni sawa. Hakuna mabepari tena, wote ni Wakomunisti." Je! ulipata kutulia na kuwazia ya kwamba huo ni uamsho wa uongo, Ukomunisti ni uamsho wa uongo? Naye aliubuni huo wote kutokana na kitu gani? Ninii . . . Yesu alisema, "Roho hizo mbili zingefanana sana, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Na kila kitu alicho nacho ibilisi, ni upotovu wa kile alichoumba Mungu. Dhambi ni—ni haki iliyopotoshwa. Uongo ni Kweli iliyowakilishwa vibaya. Uzinzi ni—ni, tendo ambalo Mungu alituamuru, likapotoshwa. Kutokuamini kote ni kupotoshwa kwa imani. Inakubidi kuikana Kweli kusudi uchukue hu—huo upotovu. Unaona, zinyoshe sauti hizi, zipime na Neno uone kama ni Kweli.

66 Loo, jinsi ambavyo tungeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi, juu ya sauti hizi za leo hii, bali wakati wetu umepita. Lakini, sauti nyingi sana hata watu hawajui la kufanya. Mmethodisti hatimaye atamsikiliza mhubiri wa Kibaptisti, wataenda kule, watakaa huko kwa muda kidogo kisha wataenda kwa la Kilutheri. Na katika Pentekoste, wana makundi mbalimbali, mmoja atakimbilia moja, na mwingine lingine, kisha kurudi na kwenda. Inaonyesha wewe huna msimamo. Isikilize Sauti Yake! Hii hapa, imeandikwa kwenye karatasi, ile Sauti, Sauti hiyo itathibitishwa kama ni Kweli.

67 Ulimwengu wa kanisa haujui la kufanya, ulimwengu wa kisiasa uko katika machafuko. Kila kitu kinaonekana kwamba kiko katika machafuko. Jamaa wanatoroka kutoka hapa, kitu kingine kinaibuka, jaketi fulani, kabuti fulani. Nilipokuwa Roma, wana misumari kumi na tisa iliyothibitishwa ambayo ilipigiliwa mkononi mwa Yesu; na kuna mitatu tu,

bali wana rekodi ya misumari kumi na tisa mbalimbali. Sasa, inaleta tofauti gani ni nani aliye na msumari huo? Kristo kamwe hakutuachia misumari tuiabudu, Yeye alituachia Roho Mtakatifu, kwa Neno Lake! “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, watakuwa na ule msumari wenyewe hasa”? “Watakuwa na. . .Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, watakuwa wafuasi wa dhehebu nililoanzisha”? Hakuanzisha lolote. Unaona jinsi sauti hiyo ilivyo kinyume?

68 Lakini, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; katika Jina Langu watatoa pepo.” Hilo hapo Neno. “Watanena kwa lugha mpya; watashika nyoka, hilo halitawadhuru. Kama wakinywa vitu vya kufisha, hakitawasumbua. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Nawe angalia mambo haya pamoja na Maandiko mengine yote yakiwekwa pamoja.

69 Sasa, hilo pekee halitalithibitisha, hata kidogo. Hapo ndipo sisi Wapentekoste tunapoingilia barabara mbaya. Hivi Yesu hakusema, “Wengi watanijia Mimi katika siku ile, na kusema, ‘Bwana, mimi sikufanya kazi kubwa katika Jina Lako? Mimi sikutabiri katika Jina Lako? Mimi sijafanya haya yote katika Jina Lako?’” Naye Yesu akasema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mnaotenda maovu, sikuwajua kamwe.” Mnaona, dada zangu na ndugu zangu, ni kwa nini ninahukumu na kukishtaki kizazi hiki? Huenda ukasema kwa lugha kama wanadamu na Malaika, huenda ukacheza katika Roho kote kanisani, hilo halina uhusiano wowote Nalo.

70 Nimewaona Waislamu wakicheza dansi wakizunguka namna hiyo. Nimesikia katika mchawi. . .kambi ya mchawi, nimewaona wachawi wakisimama na kunena kwa lugha na kuzifasiri, na kusema yale hasa yatakayotukia, na yalitukia vivyo hivyo. Nimeona hata penseli ikiinuka na kuandika katika lugha zisizojulikana, na ni mmoja tu pale angaliweza kuyasoma, naye alikuwa ni wa ibilisi. Huwezi kuwekea msingi kikomo chako cha Milele juu ya mhemuko fulani. Shetani anaweza kuiga yoyote ya mihemuko hiyo. Sio. . .Ni kumjua Kristo, kitu fulani kinabadilika maishani mwako. Yaangalie maisha yako na uyafananishe na Neno, na uone mahali ulipo. Ukifanya mahesabu, hakika.

71 Mbali na kuiga huku kote, sauti za uongo, manabii wa uongo, mambo haya mengine yote yanayoibuka, Yesu angali alisema, mbali na mambo haya yote, “Kama mtu yeyote atasikia Sauti Yangu na kunifuata Mimi.” Yeye ni Neno. Sikilizeni, agizo Lake kwetu leo, katika sauti hizi zote. Ambazo, nilisema ingechukua saa nyingi kuzielezea sauti hizi zote. Nazo zinawakanganya watu, ni jambo la kusikitisha. Na, hata hivyo, hupati nafasi ya pili, inakupasa kulichukua sasa. Huenda usipate nafasi usiku wa leo. Huenda usipate nafasi kesho. Ni sasa! “Unapoisikia Sauti Yangu, usiufanye mgumu moyo wako,

kama wakati wa kukasirisha. Wakati ndio huu. Huu ndio wakati uliokubalika kwamba kama mtu yeyote ataisikia Sauti Yangu." Hiyo inaonyesha ya kwamba Sauti Yake ingali ingekuwapo katikati ya machafuko yote. Yeye angali ana Sauti! Kwa nini? Sauti Yake itadumu daima. Hii hapa, "Mbingu na nchi zitapita, bali Sauti Yangu haitapita kamwe," Neno Lake.

72 Hebu na tuchukue tu, tuseme, dakika zingine tano, upesi. Je! mnaweza, mtakaa muda huo, ama dakika chache? Sasa, nitaharakisha. Hebu tuchukue tu wachache walioisikia Sauti hii na kuitii. Jinsi ilivyowafanya watende, kile ilichowafanya kutenda. Sasa nitaruka Maandiko me—mengi hapa, kusudi tu niwaelezee moja kwa moja jinsi ilivyoyabadilisha maisha yao na hao wote waliowazunguka, jinsi walivyofanyika wa kipekee, tunaita "wa kipekee." Kila mtu aliyepata kumwamini Mungu, alihesabiwa kuwa wa kipekee. Kwa sababu, kama uko katika mwelekeo wa ulimwengu, kuna kitu fulani kasoro kwako. Kuwa Mkristo huna budi kuwa wa kipekee. "Kwa kuwa wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo wataudhiwa na ulimwengu. Yeye alikuwa katika ulimwengu, na ulimwengu uliumbwa na Yeye, wala ulimwengu haukumjua." Upesi sasa, sikilizeni kwa makini tunapofunga.

73 Adamu aliisikia Sauti Yake, wakati wa jua kupunga, naye akafanya ushirika pamoja Naye. Hakukuwako na hukumu kwa Adamu. Yeye aliisikia Sauti ya Mungu, naye akasema, "Baba, sasa ninalala chini usingizini." Ndipo akalala chini, Naye Hawa mkononi mwake, simba, chui milia, na wanyama pori walilala moja kwa moja kumzunguka, wala hakukuwa na madhara, hakuna njia ya kupata ugonjwa, hakuna njia ya kushangaa kama angeamka asubuhi, wataamka. Adamu akaisikia Sauti Yake jinsi alivyopaswa kuisikia.

74 Lakini siku moja aliisikia sauti ya mkewe. Afadhali niliache hilo kwa muda kidogo. Bali yeye aliisikia sauti isiyo, hata hivyo ilikuwa ni mke wake, kiungo cha karibu sana alichokuwa nacho duniani. Kwa nini yeye, kama Ayubu, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu."? Na kama angalifanya hivyo, jamii yote ya binadamu wangekuwa wanaishi badala ya kufa. Ilibadilisha mwelekeo wa binadamu na wa wakati. Bali yeye aliisikia Sauti ya Mungu, alikuwa na ushirika Nayo, bali wakati alipogeuka. . . Yeye alijuaje ya kwamba mke wake alikuwa amekosea? Kumbukeni, lilikuwa ni la kupendeza.

75 Tunafiriki siku hizi ya kwamba dhehebu letu, kanisa, tunafikiri ya kwamba ufanisi wetu leo ni Mungu akitukunjulia uso. Unaonekana ni mzuri. Lilionekana ni jambo zuri wakati Mikaya aliposimama pale mbele ya manabii mia nne, na nchi nzima ilikuwa ni mali yao, nao Wafilisti waliikalia, ama Waashuri, lilionekana ni jambo zuri. Manabii hawa walikuwa wakisema, "Kwea kule, hiyo ni mali yetu. Iteke!" Bali haikuwa ni Sauti ya Mungu. Ndipo Mikaya akageuka akailaani sauti hiyo.

Naye alijuaje kufanya jambo hilo? Kwa sababu ono lake lilikuwa linalingana kabisa na Neno. Hiyo ndiyo njia tu ya kuliamini na kuliona leo, halina budi kuwa kwenye Neno.

76 Basi je! uliona baada ya Adamu kuisikiliza sauti nyingine mbali na Sauti ya Mungu, mke wake mwenyewe. Nalo kanisa linasikiliza sauti ya dhehebu lake, likiingiza ndani yake kanuni za imani badala ya Neno, likiwaacha waishi vyovyote watakavyo. Mradi tu wanaenda kanisani na ni wafuasi wa kanisa fulani, hilo ndilo tu lililo muhimu. Kiungo kilicho karibu sana mwaminio alicho nacho duniani, kwao, ni kanisa. Lakini mwaminio, mwaminio wa kweli, kiungo cha karibu sana ni Roho Mtakatifu, ni Neno la Mungu.

77 Kwa hiyo mnaona ya kwamba Adamu alitambua hali yake, ndipo akaisikia Sauti ya Mungu ikiita tena, naye alikuwa amevaa majani ya mtini wakati huo. Bali ilikuwa ni sauti ya hukumu, "Kwa nini umefanya jambo hili?"

78 Sijui kama Marekani leo, ama ulimwengu katika vurumai zake za dini, kama ilivyo, na Marekani ikimeza, ikimezwa, itakuwa ndiyo dini ya taifa karibuni. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

79 Ni nani anayekaa mbele yangu? Ninajua ni kanda nazo zitaenda kote ulimwenguni. Tuna programu za kanda, ya kwamba kila Ujumbe unasambazwa kote ulimwenguni, nchi zingine zote.

80 Vema, sasa kama utaangalia na kuona, unasimama tu katika majani ya mtini. Wakati Sauti ya kweli ya Mungu inapotokea, wao hawajui la kufanya juu ya jambo hilo. Linatatiza, hawajui la kufanya.

81 Upesi, Nuhu aliisikia Sauti ya Mungu. Ilikuwa ikijiandaa kuyaokoa maisha yake, naye aliyafuata yale maagizo naye akasimama.

82 Kama mtu akiisikia ile Sauti . . . Sasa sikilizeni, shikeni hili vizuri sana. Msikose. Kama mtu akiisikia sauti ya kitu fulani, na endapo imethibitishwa kuwa ni Sauti ya Mungu, na ni katika wakati wake, na halafu hiyo inatoka kwa mtu huyo, mbingu na nchi zitapita bali Neno hilo haliwezi kupita.

83 Nuhu aliisikia ile Sauti, naye akauhukumu ulimwengu. Nao wakamcheka usoni mwake kwa sababu Ujumbe wa—wake haukuendana na mafanikio yao ya kisayansi, bali ilinyesha na kuuangamiza ulimwengu wote. Unaona? Sauti yake iliyotoka, mbegu ilikuwa imekaa pale. Kila wakati imekuwa vivyo hivyo.

84 Samweli, alishtuka wakati alipoisikia Sauti ya Mungu, ya kwamba alikuwa . . . aende akamhukumu Eli, mtu aliyekuwa amemlea. Mtu aliyekuwa ni baba kwake na alikuwa amemlea na kumlisha.

85 Ndugu wahudumu, niendelee? Wahudumu, mara nyingi, juu ya misingi ya madhehebu yao na kanuni za imani, vitambulisho vyao mfukoni mwao, vya baba yule yule, dhehebu lile lile lililowalea na kuwalisha na kuwatunza na kuwaweka mahali pao kanisani, na kuwaweka katika kusanyiko, huna budi kushikilia yale wanayofundisha. Unaona? Lingekuwa ni jambo la kuchukiza jinsi gani kwa mtumishi wa kweli wa Mungu kuisikia Sauti ya Mungu na imbidi kurudi kwenye dhehebu lilo hilo lililomzaa, aseme, "Mmehukumiwa kwa sababu hamlikubali Neno hili." Ni jambo la jinsi gani!

Ilikuwa ni vigumu kwa Samweli. Lakini yeye alikuwa ni nabii, ilimbidi kufanya jambo hilo. Haidhuru kama liliumiza ama halikuumiza, ilimbidi kufanya jambo hilo haidhuru.

86 Musa aliisikia Sauti ya Mungu. Yeye alikuwa amejaa theolojia. Yeye alijua *habari zote*, bali hiyo ilishindwa. Aliisikia Sauti ya Mungu, Musa hakuwa yeye yule tena.

87 Na hakuna mtu anayebaki alivyokuwa kamwe. Unaweza kusikia katika masikio yako hiyo—hiyo Sauti ikinena, bali wakati unapoisikia moyoni mwako, hiyo Sauti ikinena, unaona, basi unaisikia. Wewe huoni kwa jicho lako. Unaangalia kwa jicho lako, unaona kwa moyo wako. Unaona jambo fulani, unasema, "Silioni kamwe," unamaanisha hulielewi. Husikii kwa masikio yako, unasikia kwa moyo wako. Mara nyingi masikio yako huisikia Sauti ya kweli ya Mungu, Nalo linakuangukia kama maji yakitiririkia mgongoni mwa bata. Lakini unaposikia kweli, unasikia kwa moyo wako.

88 Na theolojia yote aliyokuwa nayo Musa, hakuwa ameisikia Sauti ya Mungu. Lakini siku moja Mungu alimwita huyu mchunga-kondoo mwenye umri wa miaka themanini upande mmoja na kusema naye, naye akaishika. Alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Jambo la kwanza alilomfanyia Musa, lilikuwa ni kulithibitisha Neno Lake, "Ninashuka chini, ninakumbuka niliyoahidi."

89 Na hili ndilo aliloahidi kwa ajili ya siku za mwisho. Yeye atawainua watu kutoka katika Mataifa, na ahadi zote.

90 "Nimeahidi jambo hili." Kasema, "Musa, vua viatu vyako." Kwa maneno mengine, iheshimu Hiyo. "Sasa itupe chini fimbo yako." Na ki—kijiti kikavu kutoka nyikani kikawa nyoka, ndipo Musa akaishika, nayo ikairudia hali yake tena. Unaona? Yeye alijua huyo alikuwa ni Mungu, kwa sababu Mungu alisema, Neno la Mungu, lile Neno alilokuwa akinena, kasema, "Itupe chini fimbo iliyo mkononi mwako." Hilo ni Neno la Mungu. Usijaribu kufanya jambo lilo hilo, hilo si Neno la Mungu kwako, hilo ni Neno la Mungu kwa Musa. *Hili* hapa Neno la Mungu kwako! "Itupe chini hiyo fimbo." Ikageuka kuwa nyoka. Kasema, "Sasa unaiogopa? Ichukue kwa mkia," ndipo

ikarudi tena. Neno la Mungu kwake. Yeye alifanya nini? Mungu alithibitisha Neno Lake.

91 Nilipigiwa simu hapa miezi michache iliyopita, yapata, imekuwa, loo, imekuwa ni kama mwaka mmoja, zaidi ya mwaka mmoja uliopita. Maskini mama mmoja upande mwingine wa mawasiliano ya simu, akiwa na mhubiri Mbaptisti na mhubiri Mpentekoste. Alisema, "Ndugu Branham, Bwana amenifanya nabii mke."

Nikasema, "Sawa."

92 Kasema, "Unajua, nimeambiwa ya kwamba ulisema ya kwamba u—ulishuhudia ya kwamba huduma yangu ilikuwa ni ya Mungu."

93 Sasa, nisingefanya jambo hilo, ni kinyume cha Neno. Kwa hiyo nikasema, "Mama, hilo ni kosa. Hata sikujui."

94 Na huyo mhubiri Mbaptisti, nilimsikia, nilimsikia mhubiri huyo Mpentekoste. Huyo mama akasema, "Vema, nina mkutano hapa." Kisha akasema, "Bwana anafanya mambo makubwa."

95 Nikasema, "Ninashukuru kwa jambo hilo." Akasema . . . Nikasema, "Je! Yeye amepata kukwambia jambo lolote hadi sasa?"

Kasema, "Naam, tayari nina mpango mkubwa sana."

96 Nikasema, "Vizuri sana." Nikasema, "Sasa, mpango wako ni upi?" Nikasema, "Bwana alikwambia nini?"

97 "Yeye alisema, 'Nenda Phoenix, Arizona, tarehe *fulani*, ndipo nitakupa ule Mgodi wa Dhahabu wa Mholanzi uliopotea, nawe utaichukua dhahabu hii inayopatikana mle ndani nawe utawadhamini wamishenari kote ulimwenguni.'" Wakati sote tunajua ya kwamba ule Mgodi wa Mholanzi uliopotea ni hekaya. "Ndivyo Yeye alivyosema."

98 Nikasema, "Vema, nitakwambia jinsi ya kupata kujua kama ni Mungu ama siye." Nikasema, "Wewe uwe kule siku hiyo. Na kama kweli ukiupata huo Mgodi uliopotea wa Mholanzi, basi ni Mungu. Kama hutaupata huo Mgodi uliopotea wa Mholanzi, basi tubu na umwondolee mbali huyo pepo anayesema uwongo akutoke." Hiyo ndiyo njia ya kutafuta kujua kama ni Mungu ama siye.

99 Mungu alisema, "Musa, tupa hiyo fimbo chini, nayo itabadilika iwe nyoka." Akafanya hivyo. Akasema, "Ichukue nayo itakuwa ni kijiti tena." Akafanya hivyo.

100 Mungu anapotoa ahadi ya huduma katika siku hizi za mwisho, Yeye ataithibitisha jinsi hasa Yeye alivyosema angeithibitisha. Ndipo unajua una Sauti ya kweli. Unasikiliza Kitu halisi, kwa sababu ni Neno likithibitishwa. Unaona? Loo, jinsi . . . Samahani, mimi . . . Vema.

101 Musa alifanya tofauti. Angalia ni jambo la—la kuchekesha jinsi gani alilofanya Musa. Sasa, daima wakati unapoifuata Sauti ya Mungu, wewe ni mwenda wazimu, kwa ulimwengu. Kesho yake, Musa alijikuta, huku mke wake ameketi juu ya nyumbu, na kitoto kichanga pajani mwa mkewe, ama huo ni msamiati wa kusini, "mtoto" pajani mwake, na hao hapo. Mzee huyu akiwa na ndevu zilizoning'inia chini namna *hii*, na upara wake uking'aa, fimbo mkononi mwake, akimwongoza punda mdogo, akishuka kwenda moja kwa moja Misri upesi tu alivyoweza kwenda. Mtu fulani akasema, "Musa, ati unaenda wapi?"

102 "Ninashuka kwenda Misri, kukiteka kitu hicho." Ambapo alikuwa ameshindwa kama kijana mwanamume, alikuwa ameshindwa kama mwanajeshi, lakini huyu hapa akishuka kwenda kuiteka. Naye aliiteka. Kwa nini? Yeye alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu na kuiona ikithibitishwa kwa siku yake, kwa ajili ya yale mambo yaliyokuwa yatukie katika siku yake. Yeye aliyaona.

103 Paulo, Mfarisayo mwenye mtindo wa kibinafsi, amejaa tu theolojia alivyoweza kuwa, bali siku moja aliisikia Sauti ya Mungu. Aliiona ile Nguzo ya Moto, naye akajua ya kwamba kulikuwako na jambo fulani tofauti. Iliyabadilisha maisha yake. Haidhuru ni Mafarisayo wangapi, ni akina Gamalieli wangapi ama chochote kile wangaliweza kumpigia Paulo makelele, "umekosea, umekosea," Paulo, wakati alipoisikia Sauti ya Mungu, alijua ilikuwa ni Kweli.

104 Petro, wa kidini kama alivyoweza kuwa, akiyashika mapokeo ya wazee, asingekula nyama yoyote. La, bwana. Asingekuwa na uhusiano wowote nayo hata kidogo. Yeye kweli alikuwa akiyashika mapokeo ya wazee, kikamilifu kwa Neno. Ni jambo gani lililotukia? Siku moja aliisikia Sauti ya Mungu, "Usikiite hicho kwamba ni kichafu na ni najisi, nikiisha kukitakasa." Alikuwa ni mtu aliyebadilika. Alikuwa tayari kwenda popote alipotumwa na Bwana.

105 Nikifunga, huenda nikasema jambo hili. Kulikuwako na mtu wakati mmoja aliyekuwa ni mwaminio. Alikuwa amekufa siku nne. Alikuwa kaburini, akinuka, ameoza, bali aliisikia Sauti ya Mungu ikisema, "Lazaro, njoo huku!" Na kama ilimfufua mtu baada ya kufa na kuoza, inapaswa kufanya nini kwa kanisa ambalo lingali lina uhai ndani yake? Inapaswa kuwafufua, katika machafuko ya sauti hizi zote ambazo tumenena habari zake, za kidini, siasa, Hollywood, nabii zote za uongo na kadhalika ambazo zimeenezwa. Katikati ya haya yote, Sauti ya kweli ya Mungu itamwita mtu, ambaye amekufa katika dhambi na makosa, apate kuishi tena. Inapaswa kulichukua kanisa lililorudi nyuma na kuliita lipate uzima tena. Hakika!

106 Kumbukeni, katika kufunga, ninasema jambo hili, kisha nitafunga. Yesu alisema, “Wakati unakuja, wakati wote waliokuwa kaburini wataisikia Sauti ya Mungu.” Nawe utaisikia. Haidhuru uko katika hali gani, utaisikia kwa vyovyote vile. Na baadhi yao watakaotoka kaburini, watakuja hukumuni. Wataisikia Sauti, bali inahukumu. Na kama ukiisikia leo hii, “Leo, baada ya muda mrefu, mtakapoisikia Sauti Yangu, msiifanye migumu mioyo yenu, kama mlivyofanya katika siku za kukasirisha.” Na kama ninyi, Wapentekoste mnaofanya makundi ya kanuni za imani tena, katika mambo ya ulimwengu, “mkiwa na mfano wa utauwa na kuzikana Nguvu zake,” kabla haijakubidi kufufuka katika ule ufufuo kuhukumiwa, kwa sababu Sauti ya Mungu inayosema nawe sasa kupitia kwenye Neno itakuhukumu kwenye siku hiyo.

107 Kama wewe ni mwaminio vuguvugu tu, Sauti ya Mungu inapaza sauti moyoni mwako asubuhi ya leo, “wewe ni mwaminio vuguvugu,” afadhali utubu!

108 Wewe mwanaume, wanawake, wavulana ama msichana, ambao hammwishii Kristo, na Sauti ya Mungu inasema nanyi kupitia kwenye Neno Lake na kusema “acha kufanya jambo hilo,” afadhali ufanye hivyo. Kwa sababu utaisikia tena siku moja, Nayo itakuhukumu. Huwezi kuikana, inazungumza nawe sasa. Na, kumbuka, inarekodiwa.

109 Na wale wanaotenda mema na kuisikia Sauti Yake, watafufuka katika haki, kwa Utukufu, waende Mbinguni.

110 Kwa hiyo utaisikia Sauti ya Mungu siku fulani. Labda asubuhi hii inazungumza ndani ya moyo wako kwa sauti inayofifia, ya kwamba unapaswa kugeuka kutoka kwenye njia unayopitia, umgeukie Mungu. Sasa, kumbuka, wao watairekodi Sauti hiyo inayosema na moyo wako, huko Mbinguni. Na siku moja wakati Yesu atakapoita, na wote walio kaburini, wote, wema na wabaya, watafufuka. Na ndipo Sauti ii hii itakunong’onezea moja kwa moja tena, “Huko Phoenix, Arizona, kwenye Jumapili *fulani* asubuhi, wakati yule mhudumu alipowaweka kwa muda mrefu, akinena juu ya Sauti, Mimi nilisema nawe; niliwaambia ninyi wanawake mwache nywele zenu zikue, mwache kuvaa kizinifu; nikawaambia enyi wanaume mwachane na huko kusema uongo, kuvuta sigara; nikawaambia ninyi wahubiri kulirudia Neno la Mungu.” Mnaona ninalomaanisha? Hiyo ni kweli.

Hiyo Sauti tulivu inasema, “Huenda ikawa ni kweli.”

111 Kama ilinibidi kuja kama Nikodemo, bado ningejaribu kufika pale. Ningemjia, na kuenda huku nje jangwani mahali fulani, na kusema, “Bwana Mungu, mimi hapa, nibadilishe sasa. Nifinyange katika namna Yako.” Rudini kwenye Neno. Mahali fulani ambapo unaona ya kwamba unaliacha Neno, rudi moja kwa moja mahali hapo, kwa sababu mnyororo uko

na nguvu sana kwenye kiungo chake kilicho dhaifu sana. Na mahali popote maishani mwako ambapo umeiacha amri ya Mungu, kuyatumikia mapokeo, hapo ndipo mnyororo wako utakapovunjikia haidhuru uko imara jinsi gani kwenye jambo hilo lingine. Ushikilie mkono wa Mungu usiobadilika.

112 Na tuombe. Leo hii, baada ya muda mrefu sana, Bwana, Wewe ulisema ya kwamba utanena, ungeandika amri zako juu ya vibao vya mioyo. Sijui kilicho mbele yangu. Jambo pekee nijualo ni kulichukua Neno Lako na kulitangaza, hakika litatua chini ya miamba mahali fulani. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utazungumza na kila kijana, kila mtu wa makamu, mzee, chochote kile. Nena na moyo wangu, Bwana. Nena na mioyo ya wahudumu hawa. Nena na mioyo ya kusanyiko.

113 Tunaomba, Baba, ya kwamba leo tutaisikia Sauti Yako. Nasi tunajua, kama ilivyokuwa katika siku za Samweli, ono dhahiri ni jambo adimu, na liliwashtusha watu. Ndivyo ilivyo siku hizi. Tuna ndoto na waotaji ndoto, tuna wahubiri na wakalimani, bali ono dhahiri likitoka pamoja na Neno la Bwana, na kusahihishwa. . .Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Sauti hiyo iliyokuwa ikilia nyikani, "itengenezeni njia ya Bwana," kwamba tunaamini Roho Mtakatifu anatoa Sauti hiyo tena leo, "Jiwekeni tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana!" Na jinsi hilo lilivyo la kipekee, maana zipo sauti zingine nyingi za kuipooza Hiyo na kuiondolea mbali, bali ni ya neema katika masikio ya wale wanaoisikia. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu sasa atafanya kazi katika mioyo yetu sote.

114 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, na ninaamini mioyo yetu imeinamishwa: Kama unajua mahali fulani ambapo hujatii maishani mwako, unajua Maandiko fulani, ambayo unajua hilo ni fundisho la Biblia ambalo hujalitii, kwa sababu kitu fulani, sauti ya Hollywood ilikufanya ufanye jambo la tofauti. Mahali fulani ambapo ninyi wahudumu mmepata mahali katika Biblia, jambo ambalo hakika ni Kweli, bali mnajua dhehebu lenu lingewafukuza kama mlifundisha jambo Hilo, nanyi mnajua ni Kweli kabisa. Kwenu ninyi watu mnaokichukua kitu kibaya, mnaoishi maisha mabaya. Ninyi akina Baba na mama ambao hamjaribu kuwasahihisha watoto wenu, hamjaribu kuwalea. Huenda mkajaribu mwezavyo, nao wanaendelea kuwa wa kilimwengu kwa vyovyote vile, lakini mnaweka mfano mbele zao. Na kama hamfanyi hivyo, Sauti ya Mungu inasema nanyi, "Msifanye hivyo."

115 Na sasa huku kila kichwa kimeinamishwa na macho yote yamefumbwa, na hebu Mungu wa Mbinguni na aangalie chini kwenye mioyo ya mtu huyo anayeona njaa na wapate mahali walipokosea. Na huku amemwinulia Mungu mkono, akisema, "Bwana, hakika nina shauku ya Sauti Yako kuondoa kutokuamini kote, na mambo yote yasiyo kama Wewe, na

unifanye jinsi unavyotaka niwe," mngeinua mikono yenu. Wakati ninyi . . . Bwana abariki. Mungu akubariki.

116 Ndipo Biblia ilisema, Yesu alisema, na mbali na sauti hizi zingine zote, "Hata hivyo kama mtu ataisikia Sauti Yangu." Kumfuata Yeye, utapata unachotaka.

117 Bwana, wakati unaisha. Lakini Biblia ilisema ya kwamba, "Wote walioamini, walibatizwa." Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba kila mmoja wa hao walioinua mikono yao katika maungamo ya kweli, ya kwamba Neno la Mungu ambalo wamesoma, na kuona ya kwamba wamekuwa makosani. Kamwe sikuangalia nusu yao. Si kazi yangu kuangalia, ni kazi Yako kuangalia, Bwana. Unajua lengo na kusudi nyuma ya mkono ulioinuliwa. Wajalie, tangu saa hii, wakusudie moyoni mwao, "Tangu siku hii, na kuendelea, nitalichukua Neno la Mungu na Sauti ya Mungu, na kuifuata haidhuru itanigharimu nini." Na waweke niani mwao, wakati wakiondoka, ule wimbo wa mshairi, "Na hivi Yesu aubebe msalaba peke yake, na ulimwengu wote uwe huru? La, kuna msalaba kwa kila mtu; kuna msalaba kwa ajili yangu. Na msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba, mpaka mauti itakaponiweka huru." Ndipo basi wakati Sauti ya Mungu itakaponena, "Nitafufuka katika haki Yake, kwa maana nimeifuata Sauti Yake, Sauti ya Neno Lake." Ninawakabidhi Kwako sasa, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo.

118 Sasa wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, ninyi mkifanya maungamo yenu na ahadi yenu. Nimeshangazwa sana na mvulana mdogo anayeketi hapa, akikizungusha kichwa chake. Na ipo Sauti kwa ajili ya kanisa, "Mimi Ndimi Bwana anayeponya magonjwa yako yote." Hiyo ni Sauti kanisani. Na ninyi nyote mlio na haja ya uponyaji, na mnaishi maisha yaliyowekwa wakfu kwa kila Neno la Mungu ambapo mnajua yaliyo mema, na mna haja ya uponyaji, sijui kama mtauinua tu mkono wenu. Inua mkono wako, "Bwana, nina haja ya uponyaji." Vema.

119 Sasa, iweke Sauti hiyo moyoni mwako, "Mimi Ndimi Bwana anayeyaponya magonjwa yako yote." Kumbukeni, wakati Neno linaponenwa, halina budi kutimia. Yesu alisema, Marko 11:22, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako."

120 Sasa, kila mtu kwa njia yetu wenyewe sasa, inamisha kichwa chako, fanya maungamo yako, "Bwana, ninaamini Neno Lako. Ninaisikia Sauti Yako ikiniambia ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Nitashuka niende na kumwekea mtoto huyu mikono, kwa kuwa yeye ni mdogo sana kujua haya yote yanahusu nini, mvulana mdogo wa thamani, mwenye urefu na umri wa maskini mtoto wangu Joseph. Na ninawatakeni ninyi

nyote mwe mkiomba, mkiomba, "Bwana, ninaisikia Sauti Yako. Ninaamini."

121 Baba wa Mbinguni, tunawaleta wasikilizaji hawa Kwako kwa ajili ya uponyaji wa mwili wao. Na, Bwana, huyu hapa maskini mtoto mdogo ameketi hapa, yeye anauvutia usikivu wangu kote kote katika ujumbe, nikimwona mzazi ameketi pale amemshika jamaa huyo mdogo. Kwa sayansi ya matibabu, hakuna tumaini kwa jamaa huyu mdogo. Kuna Sauti ya Mungu inayoabiri juu ya kila kitu. Na kama kanisa hili lilivyoungana pamoja kufanya kila amri nijuayo mimi kutimiza, mengine ni Yako, Baba. Ninashuka kwenda pale na kuweka mikono juu ya mtoto yule.

122 Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninakemea jambo hili. Jalia nguvu za Mungu, uponyaji wa Mungu . . . Jalia kuwe na tofauti sana ndani yake katika dakika tano zifuatazo. Jalia wote wamjie Mungu, kwa ajili ya utukufu Wako.

123 Baba wa Mbinguni, ulitoa ahadi. Hivyo ndivyo tu nijuavyo mimi, Wewe ulitoa ahadi. Imefanywa, kama ilivyosemwa, "Kama *ukiuambia* huu," nami ninamwambia kila pepo wa maradhi ama mateso ambaye amewafunga wasikilizaji hawa, ambaye anawafunga watu hawa, kila roho wa kutokuamini, ninasema, "Waache watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo!" Sasa, tunajua ya kwamba imeandikwa, na sasa imesemwa, na itendeke, kwa ajili ya heshima na utukufu wa Mungu. Na katika Jina la Yesu Kristo linaombwa.

124 Sasa, ninyi mnaoweza kuamini, na mnaamini, haidhuru ni jambo gani linalotukia, si lazima liwe, mbegu imeanguka humo. Kile kitu fulani kidogo ndani yako, ile Sauti. Mzazi wa mtoto huyu, haidhuru mtoto huyo yuko katika hali gani, unaamini mbegu ya Mungu ilianguka moyoni mwako, ya kwamba mtoto huyo atapata afya? Ninyi wengine mnaoombeana, mmoja kwa mwingine, je! unaamini mbegu ya Mungu ilianguka moyoni mwako, "ugonjwa wangu umekwisha"? Basi umeombewa maombi ya imani, shindilia chini nguzo hiyo. Na kama Shetani akijaribu kamwe, rudi moja kwa moja, "Nikiwa nimesimama katika lile kanisa la Kihispaniola, Jumapili ile asubuhi, nilifanyiwa maombi ya imani. Naye Mungu aliahidi!" Maombi ya imani yatawaokoa wagonjwa na Mungu atawafufua. Haina budi kutimia. Je! mnaamini jambo hilo, semeni, "Amina." Mungu awabariki. Sasa nitamrudishia Ndugu Rose ibada, nadhani hapa, Ndugu Jewel Rose.

*Sauti Ya Mungu Katika Siku Hizi Za Mwisho* SWA63-0120M
(The Voice Of God In This Last Days)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 20 Januari, 1963, katika Kanisa la Apostolic huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org